

Piga Hatua Maishani

Na Elmer Murdoch

Kimetafsiriwa na
Revocatus Meza



Mungu ni Mungu wa ajabu ambaye anakupenda na amekuwa akitaka utayari wako.

*Pengine
baadhi
ya mambo
haya
yamezuia jambo
hilo
kutokea...*



Kujihusisha kwako na mambo hayo kunaweza kuwa kumekufanya uache kufikiri juu ya Mungu. Hata hivyo, utakapokuwa unasoma kijitabu hiki, Mungu anaweza kusema nawe jambo fulani.

Nukuu zote za Maandiko Matakatifu katika kijitabu hiki ni kutoka katika BIBLIA TAKATIFU.

© Copyright 1971, 1989, 2004, 2006

Pengine tayari unafahamu jambo fulani kuhusu Mungu, lakini hapa kuna mambo makuu muhimu matatu ambayo unapaswa kuyazingatia.

... Yeye ni mwenye hekima na anafahamu kipi ni muhimu kwa maisha yako.

... Yeye ni mtakatifu, hawezi kukubali dhambi na atatoa hukumu.

... Yeye mwenye rehema hivyo Anaweza kubadilisha hukumu na kukusamehe kwa kifo cha Yesu msalabani. *“Ni nani Mungu kama wewe, mwenye kusamehe uovu...”* Mika 7:18

Yesu Kristo ndiye njia pekee ya kwenda kwa Mungu, kwa kuwa anasema *“... Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.”* Yohana 14:6

Je, umewahi kujiuliza...

“Je, lengo kuu la maisha ni lipi?”

Wengine husema - kufurahi na familia yangu, kuwa mwenye furaha, kuishi maisha mema, kuridhika. Haya ni mazuri, lakini Biblia inatuambia lengo kuu ni hasa kumfahamu Mungu kwa uzoefu upatikanao kwa Yesu Kristo. Fikiri juu ya hilo! Hakika unaweza kumfahamu Mungu kama unavyoweza kumfahamu rafiki yako.

“Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.”
Yohana 17:3

Huyu Mungu wa ajabu anataka

- Kukusamehe dhambi zako zote
 - Kukupa maana katika maisha yako sasa
 - Kukupeleka peponi mara uhai wako utakapo koma

Haya yote ni yako iwapo utakabidhi maisha yako kwa Bwana Yesu Kristo.

Iwapo utakataa zawadi hii ya rehema na upendo, unajiweka mwenyewe juu ya Mungu na chini ya hukumu yake. (Yohana 3:36) Unajiweka mwenyewe kuwa mwenye mamlaka ya mwisho.


Hivyo, swali la maana sana ambalo utakuja kukutana nalo ni-

NI NANI AONGOZAYE MAISHA YAKO?

Wewe mwenyewe au Yesu? Kurasa chache zinazofuata zitakusaidia kuelewa.

Kila mtu yuko kwenye moja ya hatua hizi 5.


Msimamo wako huonyesha umbali wako kutoka kwa Mungu. Kila “hatua” huelezea hali ya moyo katika kumwelekea Mungu na hiyo huonyesha umbali wako-karibu au mbali-kutoka kwake. Yesu alifundisha haya aliposema kwa mtu aliyekuwa akitafuta ukweli, *“Wewe hu mbali na ufalme wa Mungu.”* Marko 12:34



KUTOJALI

Huenda unajua kwa kiasi cha kutosha juu ya Yesu na wokovu, au unafahamu kiasi kidogo. Jambo la msingi ni kwamba hujali.


Hali ya kutojali itakufanya uwe mbali na kumfahamu Mungu, lakini haimfanyi Mungu aache kukujali. Kwa kuwa “. . . Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.” Warumi 5:8



KUJALI

Unafhamu juu ya mahitaji yako ya ndani na ya kiroho na ungelipenda kutafuta ufumbuzi wake.

Pengine kifo, talaka, kuachishwa kazi, maradhi, au ushawishi wa rafiki umekuwezesha kugundua upweke wako au mahitaji yako ya kiroho. Upweke huu unasababishwa na kutokuwa na uhusiano na Yesu Kristo. Bwana asema, "*Nanyi mtanitafuta, na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote.*"
Yeremia 29:13



HATIA

Upo katika mahangaiko makubwa ya kiroho na kujisikia kuwa mkosaji hali inayosababishwa na Roho Mtakatifu kukuonyesha dhambi zako na upweke.

Je, unategemea kwenda mbinguni “kwa kuwa mwema” au “kwa kujitahidi kadiri ya uwezo wako?” Maswali ambayo unapaswa kujiuliza ni “Mimi ni mwema kiasi cha kutosha? Je, nimeweza kushika amri za Mungu_asilimia mia moja (100%)_ katika mawazo, maneno na matendo?” Kama umeweza, basi unaweza kwenda mbinguni kwa matendo yako mema. Mathayo 19:17-19. Hata hivyo, “. . . kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria.” Warumi 3:20



Ukitaka kujua u mwema kiasi gani, jaribu kufanya mtihamu wa Mungu juu ya wema - AMRI KUMI ZA MUNGU.

Usiwe na miungu mingine ila mimi.

Usijifanyie sanamu ya kuchonga.

Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako.

Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase.

Waheshimu baba yako na mama yako.

Usiue.

Usizini.


Usiibe.

Usimshuhudie jirani yako uongo.

Usitamani nyumba ya jirani yako.

(Kut. 20:3-17).

Umepata alama ngapi? Kufaulu ni asilimia mia moja (100%). Mungu hapimi uzani. Yakobo 2:10
“Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote.” Sheria ni kama pulizo. Tundu moja tu hutoa hewa na kuliharibu.



Kisha, jaribu kufikiri maswali haya muhimu:

1. Umepata kufanya dhambi kwa kuvunja mojawapo ya Sheria za Mungu? Ndiyo Hapana
2. Je, dhambi zako hukusumbua? Ndiyo Hapana
3. Kwa kiwango gani? Kiasi kidogo? Kiasi kikubwa? Kiasi cha kutosha kuzishughulikia?

TOBA

Una mabadiliko makubwa ya mawazo na moyo na unachagua kuzikataa na kuziacha dhambi zote zifahamikazo na haki ya kujiendeshea maisha yako wewe mwenyewe bila kumtegemea Mungu.

Toba... Ni tendo la kujivua fahari ya maisha yako ya kujitegemea mwenyewe na kumkabidhi Yesu Kristo aweze kuchukua nafasi yake halisi.

Toba... Ni kugeuka kabisa kiroho na ni lazima kabla ya kuamini.


Toba... Si suala la kuwa tu na huzuni kwa ajili ya dhambi zako. Katika toba kuna huzuni, lakini unaweza kuwa na huzuni bila hata ya kutubu. Watu wengi hujutia matokeo ya dhambi zao, lakini hawajuti juu ya dhambi yenyewe. *“Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti.”* 2 Wakorintho 7:10

Toba... Si jambo tu la kuacha matendo ya dhambi. Baadhi ya watu hujinasua kutoka katika dhambi fulani kutokana na sababu binafsi (afya, heshima, familia, biashara, nk.), si kwa sababu dhambi zao zilimchukiza Mungu.

Toba...inatajwa zaidi ya mara 55 katika Agano Jipya.

Yesu mwenyewe alisema, "Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo." Luka 13:3

Basi kutubu kuna umuhimu gani?



IMANI IOKOAYO KATIKA BWANA YESU

Umejiandaa kujitoa kikamilifu kwa jinsi ulivyo na vyote ulivyo navyo kwa ajili ya utawala wa Bwana Yesu Kristo.

Ni mabadiliko ya utawala katika moyo wako kutoka katika kujitawla mwenyewe na sasa kuwa chini ya utawala wa Bwana Yesu Kristo. Kwakuwa Kristo ni Mungu na alikufa na kufufuka kutoka kwa wafu kwa ajili yako, Yeye ni muhimu kuliko kazi yako, familia, fedha, ajira, na hata maisha yako yenyewe. Mathayo 10:37-39, Luka 9:57-62, 1 Wakorinto 15:3,4.

Katika Luka 14:26, Yesu anasema kwamba mtu akitaka kuwa mfuasi wake, lazima amtangulize Yeye kwanza kabla ya baba na mama yake, mke na watoto, nduguze. Naam, na hata maisha yake mwenyewe, ama sivyo hawezi kuwa mfuasi wake.


Unapojitua kwakwe na kumuamini Yeye kabisa, Mungu ataweka Roho yake ndani yako na utazaliwa katika familia yake. Mungu sasa anakuwa baba mwenye upendo na anaweza kufanya mabadiliko katika maisha yako kadiri atakavyo - popote na wakati wowote.

"Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka..." Matendo 16:31

“Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.” Warumi 5:1

“Alifanya amani kwa njia ya damu na msalaba Wake kwa ajili yetu.” Wakolosai 1:20

Yesu Kristo anakuwa Bwana wa maisha yako unapobadilika. Anaishi ndani yako kwa Roho wake na ni chanzo na Mwezeshaji wa maisha yako ya Kikristo.



Kwa maneno yako mwenyewe ongea na Mungu...

Tubu dhambi zako. Zitaje kwa majina:kiburi, udanganyifu,maadili mabaya,chuki, kutosamehe,nk.

Mwambie Mungu kuwa unatubu - unakusudia kuachana na dhambi zote unazozijua na chanzo cha dhambi zako ambacho ni ubinafsi.

Mwambie Mungu kuwa unamuamini Yeye tu- unajitoa kwake kabisa na kumpokea Yesu Kristo katika maisha yako kama Bwana na Mwokozi.

Atatunza ahadi yake, atakusamehe na kuja katika maisha yako, na kukufanya kuwa mpya.

Unaweza kujitoa kabisa kwa moyo wote au kwa msukumo wa nje tu.Uamuzi wako unasukumwa na dhamira, asili na jinsi Mungu akujiavyo kwako kipekee.Unafahamu kuwa umejitoe kwa dhamiri ya kweli ili kumpendeza Mungu na jambo hili ni muhimu.Misukumo ya nje itatoweka, lakini uchaguzi wa moyo wako hautabadilika.

Sasa mshukuru Bwana kwa kuwa mwana wake na kwa maisha mapya ndani yako.
Sasa unaweza kuomba.

Sababu nne za kukujulisha kuwa umeokolewa:

1 Umetii amri za Mungu kwa kutubu na kuamini, na ni Mwaminifu katika kutunza Maneno yake. *“Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele.”*
1 Yohana 5:13.

2 Una ujasiri katika damu ya Kristo iliyomwagika msalabani. *“Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake.”*
Waefeso 1:7.

3 Umeacha kujitegemea mwenyewe katika kuendesha maisha yako na badala yake umempatia Yesu Kristo, Bwana aliyefufuka, mwenye haki zote. *“Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye. . .”* Wakolosai 2:6

4 Tayari Mungu ameweka Roho wake Mtakatifu ndani yako. Katika roho yako mwenyewe anakuhakikishia kuwa u wake. *“Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu. . .”* Warumi 8:16

Maisha mapya katika Yesu Kristo huleta mabadiliko haya...

- 1. Haja ya kutaka kulijua Neno la Mungu katika Biblia.** *“Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ila kwa hayo mpate kuukulia wokovu. . .”* 1 Petro 2:2
- 2. Haja ya kumtii Yesu Kristo.** *“Mkinipenda mtazishika amri zangu”* Yohana 14:15
- 3. Kusikitishwa na dhambi.** Hatuwezi kufurahia dhambi tena. *“Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye muhuri hii, Bwana awajua walio wake. Na tena, Kila alitajaye jina la Bwana na auache uovu.”* 2 Timotheo 2:19
- 4. Kuwatafuta waliopotea.** Wale ambao bado hawaja tubu na bado hawajamfahamu Mungu kibinafsi. *“... bali huvumumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote wafikilie toba.”* 2 Petro 3:9

Kwa kuagiza nakala zaidi za kijitabu hiki wasiliana na:

Mch. Revocatus Meza

S.L.P 1104,

Mbeya,

TANZANIA.

Au wasiliana na:

Simu: 255 744 993 860; Barua-pepe: revocatusmz@yahoo.com / sutmail@aol.com ; Tovuti: www.stepuptolife.com
